

Maswali

1. Kulikuwa na wanawali wangapi?
2. Walijua wakati Bwana arusi atakuja?
3. Mbona walitakiwa wawe na taa?
4. Wanawali wenye busara walifanya nini?
5. Mbona wanawali wengine walikuwa wapumbavu?
6. Nini ilifanyika walipokuwa wakingoja?
7. Taa zilifanya nini wakati walikuwa wakimngoja?
8. Wanawali gani walijitayarisha kwenda harusini?
9. Wanawali wapumbavu walifanya nini?
10. Bwana arusi alisema nini?
11. Tunajifunza nini kutoka kwa hii hadithi?

Majibu

1. Kulikuwa na wanawali kumi.
2. Hawakujua wakati bwana arusi atakuja.
3. Walitakiwa wawe na taa wakimulikia bwana arusi njiani.
4. Wanawali wenye busara walileta akiba ya mafuta.
5. Wanawali wapumbavu hawakuleta mafuta ya akiba.
6. Wote walilala walipokuwa wakingoja.
7. Taa zao zilizima kama wangali wanangoja.
8. Wanawali wenye busara walikuwa tayari.
9. Walienda kununua mafuta.
10. “Simjui nyinyi. Wale waliokuwa tayari ndio wanaweza kuja ndani.”
11. Tunatakiwa kukesha tuingoja Yesu atupate tu tayari.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 1



43 Wanawali kumi

Marejeo

Mathayo 25: 1—13

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba tujitayarishie kurudi kwa Kristo

Maneno maalum

1. Arusi + wanawali kumi + taa.
2. Watano wa busara + mafuta ya akiba + watano wapumbavu + hakuna mafuta ya akiba.
3. Bwana arusi + taa zimezima + hakuna mafuta + enda nunua.
4. Watano wenye busara + taa zinawaka + arusi + furaha.
5. Gongu + sha chelewa + simjui nyinyi + lazima kujitayarisha

43.1 Je, umewahi kwenda arusini? Inafurahisha sana tena unakuwa ni wakati wa furaha. Fundisho hili linahusu arusi na kuhusu wanawali kumi ambao walitakiwa kuhusika katika arusi. Arusi ilikuwa inakwenda kufanyika. Wanawali kumi iliwapasa wawepo na wote walifurahi sana. Bwana arusi angefika muda maalum na ndipo wote wangekwenda pamoja na bwana arusi ili kuwasha taa zao wamumlikie njia anapopita. Muziki na kucheza vinakuwepo na kila mtu anakuwa ni mwenye furaha.

Lakini wanawali huwa hawafahamu bwana arusi anafika wakati gani. Mara nyingi inawapasa kumsubiri muda mrefu sana, na huwa wanakuwa tayari kuwasha taa zao mara tu bwana arusi anapofika.

43.2 Wote wanakuwa wamevaa mavazi mazuri maalum ya arusi, wanakuwa wameweka maua kuzunguka vichwa vyao nakila mmoja anakuwa na taa ili kumumlikia njia bwana arusi anapopita. Wanawali watano walikuwa wenye busara na walikuwa wamekuja na mafuta ya akiba ikiwa itabidi kusubiri kwa muda mrefu. Lakini wanawali wengine watano walikuwa ni wapumbavu na hawakuwa wameleta mafuta ya akiba.



Na walipokuwa wanasubiri kwa furaha walizungumza kuhusu arusi. Hata ikawa baada ya mda mrefu walichoka kuzungumza. Bwana arusi alikuwa hajafika. Walikaa chini wakapumzika, na taa zao zikiwa zimewekwa tayari kutumia kwa upande wao.

43.3 Bwana arusi alipokawia ndipo na wanawali hawa wakalala usingizi mzito sana mmoja mmoja. **Ndipo 'waliposikia kelele za shangwe!' "Bwana arusi anakuja, nendeni nje mkamlaki."** Na wanawali wote wakaamka. Wale wanawali watano wapumbavu wakasema, **"Aa! Taa zetu zinazimika. Tupatieni mafuta yenu kidogo."** **"Wale watano wenye busara wakawajibu 'Hapana' maana hayatatutosha sisi na ninyi. Nendeni haraka sasa hivi mkanunue mafuta."** Ndipo wale wanawali wapumbavu wakashika njia kwenda kutafuta mahali ili wanunue mafuta.

43.4 Kisha wale watano wenye hekima wakaondoka kwa furaha kumlaki bwana arusi. Alikuwa akiwa amevaa mavazi ya arusi na wale wanawali watano wakaziwasha taa zao sana kumumlikia njia bwana arusi na wakaenda kwa furaha pamoja naye akaingia arusini. Na wote waliokuwa tayari walipokuwa ndani mlango ukafungwa. Na wote wakafurahi maana kulikuwa muziki na kucheza.



43.5 Baada ya muda kupita mlango ukagongwa sana. Wale wanawali watano wapumbavu walikuwa wamerudi, wakasema, **"Uturuhusu tuingie ndani," "Tufungulie mlango."** Lakini walikuwa wamechelewa Sauti kutoka ndani ilisema, **"Siwajui ninyi." "Ni wale walio tayari ndiyo wanaweza kuwa pamoja nami katika arusi yangu."**